



# Nishani ya mamalia.

Nishani hii ipo katika kundi la viumbe vya asili, huwakilishwa kwa rangi nyeupe





By: Yusuph Mwasiposya

## utangulizi

- Mamalia ni mnyama mwenye uti wa mgongo na aliye na uwezo wa kunyonyesha.
- Kuna zaidi ya aina 4,000 za mamalia.
- Wengi wa mamalia hawa huishi ardhini, na wachache wao huishi majini.
- Kuna mamalia wengine huweza kuishi majini na nchi kavu, mfano kiboko.

2


## Tabia za wanyama

- Wana damu moto (warmly blooded)
- Wana vinyweleo (hairy or fur)
- Wana tezi zitoazo maziwa (milk producing glands).
- Wana tezi zinazotengeneza fati (fat-secreting glands).
- Moyo wa mamalia una vyumba vinne.

3

## Tabia za wanyama


- Mapafu ya mamalia yana diapramu inayomsaidia mamalia kupumua.
- Wana meno aina mbalimbali ndani ya midomo yao (heterodont dentition)



4

## Tabia za wanyama

- Moyo wa mamalia una vyumba vinne.




5

### Baadhi ya mamalia na sifa zao

Chiroptera

- Hawa ni Wanyama warukao ambao ni POPO.
- Kuna aina kuu 2 za popo
  1. Popo wakubwa {Megabat Megachiroptera (megabats)}
  2. Popo wadogo {Microbat Microchiroptera (microbats/echolocating bats)}
- Miongoni mwa tofauti yao kubwa ni kwamba popo wakubwa hula sana mimea, wakati popo wadogo hula sana wadudu, Wanyama wadogowadogo na samaki.


Popo mdogo



Popo mkubwa

## Baadhi ya mamalia na sifa zao

Carnivora

- Hawa ni Wanyama walao nyama.
- Wana meno yaliyochongoka (canine teeth).
- Macho yao ni makini sana.
- Wana hisia nzuri sana katika kunusa.
- Wana ubongo wenye uwezo mkubwa.
- Wana uwezo mzuri wa kuwinda.
- Lakini pia baadhi yao hawala nnyama. Mf: Panda yeye hula mianzi



Tiger

Panda




## Baadhi ya mamalia na sifa zao

Rodentia

- Hawa ni Wanyama wadogo pia.
- Wana meno yanayokua wakati wote hivyo wanatakiwa kuyasaga ili yasiendelee kukua, ndio maana wakati wote utawaona kana kwamba wanatafuna.
- Meno yao hutumika kukatia miti, kung'atia ngozi za matunda na kujikinga wenyewe.
- Rodents wana meno mawili makubwa katika taya la juu
- Rodents hula mimea na baadhi hula wadudu au samaki.
- Wana mmeng'enyo wa kujirudia kwa chakula wanachokula.



Panya kwa aina zake



## Baadhi ya mamalia na sifa zao

Lagomorpha

- Hawa ni Wanyama wadogo pia.
- Tofauti kati ya Wanyama hawa na Wanyama wengine wadogo (rodents) ni

i. Wana meno manne ya kuchania katika taya la juu, wakati rodents wana meno mawili.
ii. Hula mimea tu, wakati Rodents hula mimea na baadhi hula wadudu au samaki.
iii. Wana mmeng'enyo wa kujirudia kwa chakula wanachokula.



Sungura



## Baadhi ya mamalia na sifa zao

Cetacea

- Kuna zaidi ya aina 90 ya Cetacea.
- Wana miili kama samaki na miguu yao ya mbele ni kama vibawa.
- Kwa kawaida Cetacea ni Nyangumi
- Wana zaidi ya meno 100
- Wao hula samaki, ngisi, seal na nyangumi wenzao.





## Baadhi ya mamalia na sifa zao

Sirenia

- Kuna zaidi ya aina nne za Sirenia.
- Miguu yao ya mbele ni kama mabawa yaliyotengenezwa ili kuogelea.
- Hawana miguu ya nyuma lakini wana mkia.





## Faida za mamalia.

i. Popo hula wadudu waharibifu.
ii. Mbwa hutoa ulinzi kwa binadamu na huongoza vipofu.
iii. Paka hupunguza panya na kupunguza uwepo wa nyoka.
iv. Fisi ni msafisha mazingira na hivyo hufanya pori kuwa safi.
v. Husaidia kutupatia mbolea kutoka kwenye kinyesi chake.
vi. Ni chanzo cha mapato, kwa kuuzwa, au utalii.
vii. Punda, farasi, mbwa na ng'ombe huweza kutumika katika usafiri.
viii. Baadhi ya mamalia ni chakula kwa binadamu.
ix. Hutoa malighafi za viwanda. Mf: ngozi, kwato na mifupa hutumika kutengenezea vitu mbalimbali.
x. Hufunua ukuu wa Mungu katika uumbaji wa Wanyama aina mbalimbali.

(Taja faida nyingi kadri uwezavyo kufikiri)

12

## Hasara(madhara) za mamalia.

i. Kicheche hufanya mazingira yanayomzunguka kunuka vibaya sana.
ii. Simba, chui , dubu na mbweha huweza kuwadhuru wanadamu na mifugo.
iii. Panya hula kiasi kikubwa sana cha nafaka na kusababisha hasara kwa binadamu.
iv. Panya huweza kusababisha magonjwa kama vile Tauni.
v. Paa anaweza kusababisha ugonjwa wa chronic wasting.
vi. Wanyama wakiwa wengi husababisha uchafuzi wa mazingira, mmomonyoko wa udongo, na kuharibu misitu na umbijani.

(Taja hasara nyingi kadri uwezavyo kufikiri)


13

## Mamalia mkubwa kuliko wote duniani

- Nyangumi wa samawi (Blue Whale) ndio mamalia mkubwa kuliko wote duniani.
- Ana urefu wa mita 30.
- Ana uzito wa tani 90, hii ni sawa na kilogramu 90,000.
- Wanapatikana katika bahari zote.
- Nyangumi mkubwa ana uwezo wa kula tani 4 kwa siku, hii ni sawa na kilo 4,000 kila siku.
- Nyangumi hawa hunywa maji lita 400 kwa siku.
- Kwa sababu ya mwanadamu, leo hii Nyangumi hawa wanakaribia kutoweka kabisa duniani.
- Nnyangumi waliopo leo ni kama 1% ya Nyangumi waliokuwepo miaka 100 iliyopita.

14

## Mamalia mkubwa kuliko wote duniani




15

## Mahitaji muhimu ili kukamilisha nishani hii

- Tambua Wanyama nane waliopo katika mazingira yako.
- Tumia angalau masaa maatano katika kuwachunguza Wanyama wa porini katika mazingira yao.
- Kama hakuna pori karibu waweza kwenda katika hifadhi yoyote ya Wanyama iliyo karibu nawe.
- Andika insha ya ukurasa mmoja ukieleza yale uliyoyaona katika matembezi yako.
- Simulia kisa chochote kinachohusu mnyama au Wanyama unachokifahamu.

16

## MAMALIA KATIKA BIBLIA.

1. Mwanzo 1:20-23 – Wanyama wa majini waliumbwa siku ya tano.
2. Mwanzo 1:24-31 – Wanyama wengine waliumbwa siku ya sita kasoro Wanyama wa majini.
3. Walawi 11:4-8 - Mungu alitoa sifa za Wanyama wanaotakiwa kuliwa na Wanyama wasiotakiwa kuliwa.
4. Mwanzo 7:2-3 – Mgawanyiko wa Wanyama walio safi na walio najisi ulianza hata kabla ya gharika.
5. Waebrania 9:11-14 – Wanyama waliokuwa wakitolewa kafara wakati wa agano la kale walimwakilisha Kristo ambaye ni mbeba dhambi za ulimwengu.
6. Yohana 1:29 – Yesu hufananishwa na mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu.

17

## MWISHO:

Nishani hii ipo katika kundi la nishani za viumbe vya Sali, huwakilishwa kwa rangi nyeupe.



18